WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

# JARIDA MAALUM

TOLEO LA MWEZI OKTOBA, 2022

MATOKEO YA SENSA YA SITA
TANZANIA
SENSA
2022




Matokeo ya Sensa Dira Sahihi ya Maendeleo ya Miundombinu

## BODI YA WAHARIRI:

**Mwenyekiti**
Segolena Francis / Christopher Philemon

**Wajumbe**
Shukuru Senkondo
Biseko Ibrahim
Deniza Cyprian

**Msanifu**
Bolgas Odilo

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi
S.L.P 2888 Ujenzi/S.L.P 638 Uchukuzi
**Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma.**

Simu: +255 26 23244455
Barua pepe: ps@mow.go.tz

Tufuatilie katika kurasa zetu kwenye mitandao ya kijamii
wizarayaujenzinauchukuzi www.mwt.go.tz




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa na Mwakilishi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika Dr. Patricia Laverley, pamoja na viongozi wengine wa Serikali akifungua kitambaa kuashiria ufunguzi rasmi wa uwekaji wa jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, jijini Dodoma.*








*Viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali wakifurahi jambo mara baada ya hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, jijini Dodoma.*











# PROF. MBARAWA: MAGARI RUKSA KUPITA DARAJA LA WAMI.

Na **Christina Seggu** - WUU

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa ameruhusu Magari kuanza kutumia daraja jipya la wami kufuatia Ujenzi wake kukamilika.




Profesa Mbarawa amewataka viongozi na wananchi wa mkoa wa Pwani, Kuhakikisha daraja hilo linalindwa ili kudumu kwa zaidi ya miaka 120 iliyokusudiwa kutumika.

“daraja limekamilika kwa asilimia 96 hivyo madereva na watumiaji wa daraja hili, tumieni kwa uangalifu na kulitunza kwa kuwa kazi ndogo ndogo za ukamilishaji zikiendelea.” amesema Prof.Mbarawa.

Aidha, Prof. Mbarawa amewataka viongozi kutoa ushirikiano kwa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) na wakandarasi wanaojenga barabara ya magari yaendayo haraka ya Kibaha-Chalinze-Morogoro Express Way (km 215)Ili kuwezesha Ujenzi kuanza kwa wakati.

“Serikali inaendelea kuufungua mkoa wa Pwani kwa kuendeleza Ujenzi wa barabara kutoka Pangani - Horohoro - Lungalunga hadi Mombasa nchini Kenya ambayo itaboresha uchumi wa viwanda na kukuza utalii katika eneo hilo la kimkakati,” ameongezea Profesa Mbarawa.

Kwa Upande wake Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Eng. Dorothy Mtenga, amesema zaidi ya shilingi bilioni 75 zimetumika katika Ujenzi wa daraja hilo lilokusudiwa kutatua changamoto za daraja la mwanzo ambalo lilikuwa halikidhi mahitaji ya magari yanayopita kwa kuwa lilijengwa miaka 63 iliyopita na lilikuwa na njia moja.

Naye Mkuu wa Wiaya ya Bagamoyo, Bi Zainabu Abdalah Issa, ameishukuru Serikali hususani Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa utekeleza wa miradi ya miundombinu ya kimkakati katika Mkoa wa Pwani, inayochochea maendeleo ya Viwanda, Utalii na Biashara.


Aidha, amemhakikishia Waziri Mbarawa, kuwa madaraja na barabara zinazojengwa katika mkoa wa Pwani, zitatunzwa vizuri.

Kwa upande wake Mbunge wa Chalinze ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Ridhiwani Kikwete, ameishukuru Serikali kwa kuendeleza miradi ya miundombinu katika mkoa wa Pwani ili kurahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo.

Daraja jipya la Wami, lenye urefu wa mita 513.5, upana mita 11.85 na barabara unganishi km 3.8 linaunganisha mkoa wa Pwani na Tanga, litachochea ustawi wa jamii kiuchumi na kuleta maendeleo kwa mikoa ya kaskazini mwa Tanzania.



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa akizungumza na Wananchi wa Chalinze (hawapo pichani), mara baaada ya kukagua na kuruhusu matumizi ya Daraja la Wami Mkoani Pwani.*





*Sehemu ya Wananchi wa Chalinze wakimsikiliza Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa (hayupo pichani), mara baaada ya Waziri huyo kukagua na kuruhusu matumizi ya Daraja la Wami Mkoani Pwani.*



# DARAJA LA GODEGODE KUANZA KUJENGWA - DISEMBA.

Na **Bolgas Odilo** - WUU

Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya amesema darala la Kinyasungwi - Godegode lenye urefu wa mita 154, linalounganisha jimbo la Mpwapwa na Kibakwe mkoani Dodoma litaanza kujengwa ifikapo mwezi Disemba mwaka huu.



*Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (wa kwanza kushoto) akitoka kukagua ujenzi wa daraja wilayani Mpwawa, jijini Dodoma. Daraja hilo linaunganisha wilaya hiyo na wilaya ya Kongwa.*

Akizungumza mara baada ya kukagua barabara ya Mpwapwa-Gulwe-Kibakwe yenye urefu wa Km 48.1 Eng. Kasekenya amesema Serikali inatambua umuhimu wa daraja Kinyasungwi-Godegode katika barabara hiyo kiuchumi na kijamii hivyo ujenzi wa daraja hilo utaendana na ujenzi wa barabara unganishi za lami zenye urefu wa Kilomita 6.

"Barabara hii ni muhimu kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na ni kiunganishi kizuri cha mikoa ya Dodoma-Morogoro hadi Dar es Salaam hivyo kukamilika kwake kutaibua fursa za maendeleo kwa wakazi wa Wilaya ya Mpwapwa", amesema Eng. Kasekenya.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri Kasekenya amemtaka mkandarasi Mtwivila Traders anayejenga madaraja madogo katika barabara ya Kongwa-Mpwapwa yenye urefu wa KM 49.19 na mkandarasi Technics Constructions Group anayejenga daraja la Mpwapwa kuhakikisha yanakamilika kabla ya mvua za masika ili kuepusha athari katika madaraja hayo.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), mkoa wa Dodoma Eng. Salehe Juma amemhakikishia Naibu Waziri Kasekenya kuwa wamejipanga vizuri na ujenzi wa madaraja hayo na barabara unganishi utakamilika kwa wakati na ubora uliokusudiwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa Josephat Maganga amesema kukamilika kwa madaraja hayo kutaondoa adha wanayoipata wananchi hususan wakati wa mvua kubwa na kuboresha ustawi wa maisha ya jamii katika eneo hilo.

# MWAKIBETE AWATAKA AQRB KUONGEZA USAILI WATAALAM WA MAJENGO.

Na **Segolena Francis** - WUU

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Atupele Mwakibete, amezungumzia umuhimu wa Bodi ya Usajili Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), kuongeza idadi ya wataalam wa fani hiyo waliosajiliwa nchini.



*Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Atupele Mwakibete, akizungumza na Msajili wa Bodi ya Wabuifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Qs. Edwin Nnunduma (kushoto), wakati alipokuwa akikagua mabanda katika mkutano wa tatu wa mwaka wa watalam hao, mkoani Dar es Salaam.*

Akifungua mkutano mkuu wa tatu wa AQRB jijini Dar es Salaam Mhe. Mwakibete amesema Serikali itaendelea kutoa ufadhili wa mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu wa fani hiyo kila mwaka ili kuongeza idadi ya wataalamu hao wenye sifa nchini na hivyo kuwawezesha kufanyakazi ndani na nje ya nchi.

"Serikali inatambua na kuthamini mchango wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kwa uchumi na maendeleo ya nchi hivyo simamieni kikamilifu sekta ya majenzi ili kuboresha miji na kuleta usalama wa majengo,"

Mkutano huo unaoongozwa na mada kuu inayosema "uhifadhi wa majengo kwenye miji ya Afrika kwa sasa" unahudhuriwa na wataalamu mbalimbali katika sekta ya ujenzi kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kupeana mbinu za kuhakikisha ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi unakwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mwakibete amewahakikishia wataalam hao kuwa Serikali itaendelea kutoa ufadhili huo ili kuongeza idadi ya wataalamu wazawa na kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23 Wizara imeidhinisha kiasi cha Shilingi milioni 550 kwa ajili ya Mpango wa Mafunzo ya Wahitimu kwa Vitendo (EAPP).

Naibu Waziri Mwakibete ametoa wito kwa Bodi hiyo kuziangalia upya gharama za usajili wa wanachama ili ziwe nafuu na hivyo kuwawezesha wataalam wenye sifa kusajiliwa na kuwawazesha wananchi kutumia huduma za wataalam waliosajiliwa.





*Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Atupele Mwakibete, akitizama moja ya kazi wanazozifanya Wabuifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wakati alipotembelea mabanda yaliyopo katika mkutano wa tatu wa mwaka wa watalam hao, mkoani Dar es Salaam. Mkutano huo umeandaliwa na Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB).*



*Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Atupele Mwakibete, akihutubia washiriki wa mkutano wa tatu wa mwaka wa Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) (hawapo pichani), wakati alipofungua mkutano huo mkoani Dar es Salaam*

Mwakibete amesema kuanzia sasa wataalamu wote watahusishwa katika miradi ya ujenzi na kwamba wizara yake imeunda timu maalumu kwa ajili ya kupitia miradi inayoendelea na kutathmini mahitaji yanayotakiwa.

"Kuanzia sasa lazima wataalamu wote washirikishwe kwenye miradi, Serikali itatumia wataalamu katika sekta zote ili kukidhi mahitaji ya makundi yote," amesema Mwakibete.

"Natoa rai kwa waendelezaji kuhakikisha wanatumia wataalamu katika miradi ya 'force account'. Serikali tunaamini kwamba force account inapunguza gharama kwa Serikali, kwa hiyo hata nyinyi hamtakiwi kutupa tofauti kubwa," amesema Mwakibete.

Mwenyekiti wa Bodi ya AQRB, Dkt. Ludigija Bulamile, amesema kuna umuhimu wa kushirikisha wataalamu wote katika utekelezaji wa miradi ili kuondoa changamoto zinazojitokeza baada ya kukamilika kwa miradi husika.

Amesema miradi yote inatakiwa kuwa na wataalamu wote, wakiwamo wahandisi, wakandarasi na wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi ili kuzingatia mahitaji ya makundi yote yatakayotumia miundombinu.
Dkt. Bulamile amesema mada zitakazowasilishwa kwenye mkutano huo zitajielekeza kwenye umuhimu wa kuhifadhi majengo na kwamba majengo ya serikali yanatakiwa kuishi kuanzia miaka 60 hadi 99.

Awali, akizungumza kwenye mkutano huo, Msajili wa Bodi ya AQRB, Qs. Edwin Nnunduma, amesema Bodi hiyo imesajili wataalamu 1,329, kati yao, 1,295 ni wazawa na 34 ni wageni.

Amesema mwaka jana waliweka lengo la kusajili miradi 1,000 lakini waliweza kusajili miradi 1,097 yenye thamani ya Sh4.5 trilioni.

Kuhusu wahitimu katika fani hiyo, Nnunduma amesema takribani wahitimu 250 wanahitimu masomo yao kila mwaka, lakini ni 150 pekee ndiyo wanajiunga na bodi hiyo na kupata fursa ya kupata mafunzo kwa vitendo kwenye taasisi mbalimbali za umma na binafsi.



*Msajili wa Bodi ya Wabuifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Qs. Edwin Nnunduma*

# UJENZI WA JENGO LA ABIRIA KIWANJA CHA NDEGE CHA SONGWE WAFIKIA ASILIMIA 68.

Na **Deniza Cyprian - WUU**



*Muonekano wa hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Songwe ambapo hadi sasa umefikia asilimia 68. Jengo hilo litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 600 kwa wakati mmoja.*



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa akitoa maelekezo kwa Meneja wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe, Eng. Danstan Komba (mwenye reflector) na Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Eng. Matari Masige mara baada ya kukagua hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa jengo la abiria katika kiwanja hicho Mkoani Mbeya.*



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (mwenye kofia nyeusi) akimsikiliza Meneja wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe, Eng. Danstan Komba kuhusu hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa jengo la abiria katika kiwanja hicho wakati Waziri huyo alipokagua maendeleo yake Mkoani Mbeya.*



# BARABARA YA KIDATU - IFAKARA KUKAMILIKA MEI.

Na **Shukuru Senkondo** - WUU

Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya amemtaka Mkandarasi Reynolds Construction Company Nigeria ltd, anayejenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kidatu-Ifakara yenye urefu wa KM 66.9 pamoja na daraja la Ruaha Mkuu lenye urefu wa mita 130, kuhakikisha ujenzi huo unakamilika mwezi Mei mwakani.



*Muonekano wa barabara ya Kidatu - Ifakara KM 66.9 katika hatua mbalimbali ambayo ujenzi wake kwa kiwango cha lami unaendelea mkoani Morogoro.*

**Changamoto zote zilizokuwa zikichelewesha mradi huo zimepatiwa ufumbuzi hivyo kazi iliyobaki ni kwa Mkandarasi kukamilisha ujenzi.**

Akizungumza mara baada ya kukagua ujenzi huo Eng. Kasekenya amesema barabara hiyo itakuza kilimo katika mkoa wa Morogoro na ukanda wa kusini mwa Tanzania, kupunguza muda wa usafiri na gharama za kusafirisha mazao na pembejeo za kilimo, kuongeza thamani ya mazao na hivyo kukuza uchumi wa wananchi kwa ujumla.

"Lengo la Serikali ni kuhakikisha tunaufungua mkoa wa Morogoro ambao ni ghala la chakula ili kuunganisha kwa njia fupi na mikoa ya Njombe na Ruvuma," amesema Naibu Waziri huyo.

Amemtaka msimamizi wa mradi huo, Kitengo cha Uhandisi Ushauri cha TANROADS (TECU), kuhakikisha maeneo yote yanayohitaji kuboreshwa ili kuimarisha usalama katika barabara hiyo yanafanyiwa kazi haraka na kwa viwango.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Morogoro Eng. Lazack Kyamba amesema mradi huo ambao umefikia asilimia 68 uko katika hatua nzuri na watamsimamia mkandarasi ili ukamilike kama ilivyopangwa.

Barabara ya Kidatu-Ifakara KM 66.9 ni sehemu ya barabara ya Mikumi-Ifakara yenye urefu wa KM 130 inayopita katika ukanda wenye uzalishaji mkubwa wa mazao hivyo kukamilika kwake kutaboresha ustawi wa jamii kwa kukuza uchumi wa watu na taifa kwa ujumla.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri Kasekenya amekagua na kuridhishwa na ujenzi wa barabara ya Dumila –Kilosa- Mikumi KM 142, sehemu ya Rudewa-Kilosa KM 24 ambayo inajengwa na wakandarasi wazawa na kuwataka waongeze bidii ili kujenga imani kwa Serikali.





*Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya akifafanua jambo kwa wakazi wa Mang'ula (hawapo pichani), alipokagua ujenzi wa barabara ya Kidatu-Ifakara KM 66.9 ambayo ujenzi wake kwa kiwango cha lami unaendelea mkoani Morogoro.*

Kampuni hiyo ya Umoja-Kilosa JV inajumuisha kampuni saba za kihandisi za wazawa ikiwa ni mkakati wa Serikali wa kuwajengea uwezo wakandarasi wazawa ili kumudu kujenga miradi mikubwa na hivyo kunufaika kiuchumi na kiuzoefu.

"Barabara hii ya Dumila-Kilosa-Mikumi inayopita nje ya mbuga ya wanyama ya mikumi itakapokamilika itapunguza msongamano wa magari katika barabara ya Morogoro-Iringa na kupunguza ajali za magari kugonga wanyama katika mbuga hiyo," amesema Eng. Kasekenya.

Msimamizi wa mradi huo Eng. Protas Mwasyoke amesema wamejipanga kuhakikisha sehemu iliyobaki ya kuunganisha kwa lami barabara ya Dumila-Rudewa –Kilosa inakamilika ifikapo Machi mwakani.

Naibu Waziri Kasekenya yuko katika ziara ya siku tatu mkoani Morogoro kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara za lami.



*Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Morogoro Eng. Lazack Kyamba akifafanua jambo kwa Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya alipokagua ujenzi wa barabara ya Kidatu-Ifakara KM 66.9 ambayo ujenzi wake kwa kiwango cha lami unaendelea mkoani Morogoro.*

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU YAPOKEA TAARIFA YA MIRADI YA MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA (TPA) NA KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI (MSCL) JIJINI DODOMA.

Na **Biseko Ibrahim** - WUU



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akitoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wakati kamati hiyo ilipopokea taarifa ya miradi ya maendeleo ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) jijini Dodoma. Kulia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mhe. Anne Kilango.*



*Sehemu ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wakifuatilia wasilisho la taarifa ya miradi ya maendeleo ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) iliyowasilishwa kwao, jijini Dodoma.*





*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akiwasilisha taarifa ya awali kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wakati kamati hiyo ilipopokea taarifa ya miradi ya maendeleo ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) jijini Dodoma.*



*Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mhandisi Juma Kijavara akitoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wakati kamati hiyo ilipopokea taarifa ya miradi ya maendeleo ya Mamlaka hiyo, jijini Dodoma.*



*Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete akizungumza na Katibu Mkuu wa Uchukuzi Gabriel Migire kabla ya kuwasilishwa taarifa ya miradi ya maendeleo ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na Kampuni ya Huduma Za Meli (MSCL) kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Eric Hamissi akitoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wakati kamati hiyo ilipopokea taarifa ya miradi ya maendeleo ya taasisi hiyo, jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa akitoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu wakati kamati hiyo ilipopokea taarifa ya miradi ya maendeleo ya Mamlaka hiyo, jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mhe. Anne Kilango akitoa maelekezo kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, wakati kamati hiyo ilipopokea taarifa ya miradi ya maendeleo ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na Kampuni ya Huduma za Meli (Mscl), jijini Dodoma.*

# MKOA WA TABORA NA KIGOMA KUUNGANISHWA KWA BARABARA ZA LAMI.

Na **Siti Said** - WUU

Serikali imewaahidi wakazi wa Mkoa wa Tabora na Kigoma kuunganisha mikoa hiyo kwa barabara za lami ifikapo mwakani 2023.



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (kulia) akimsikiliza Mhandisi Mshauri wa Kampuni ya Norplan Mhandisi Henry Ngogoro (kushoto), hatua za ujenzi wa barabara ya Malagarasi – Ilunde - Uvinza (km 51.1), inayojengwa kwa kiwango cha lami, Mkoani Kigoma. Katikati ni Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Kigoma, Mhandisi Ngoko Mirumbe.*

Akizungumza kwa nyakati tofauti mkoani Kigoma na Tabora wakati alipokagua miradi iliyobakia kuunganishwa mikoa hiyo .

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa, amesema ujenzi wa barabara ya Malagarasi - Ilunde - Uvinza (km 51.1) na Kazilambwa - Chagu (km 36) kwa kiwango cha lami ni azma ya Serikali ya kuunganisha barabara zote za Mikoa na kuchochea shughuli za kibiashara katika mikoa hiyo na mikoa jirani pamoja na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi.

"Serikali inayoongozwa na Mama Samia inaendeleza Sera ya Ujenzi kwa kuhakikisha mikoa na wilaya zinaunganishwa kwa njia ya barabara bora sambamba na miradi mingine ya uchukuzi ikiimarishwa ili kumpa uhuru mwananchi achague usafiri atakaouweza", amefafanua Waziri Prof. Mbarawa.

Waziri Mbarawa amesema Serikali haitaongeza muda wa ziada kwa miradi hiyo miwili na hivyo kumtaka Mkandarasi Kampuni ya STECOL Cooperation anayejenga barabara hizo kukamilisha kwa wakati na viwango.

"Serikali haitaongeza muda wa ziada kwa miradi hii tunataka miradi hii iwe imekamilika na wananchi wafaidi matunda ya kodi wanazolipa sababu fedha tayari mmeshalipwa hivyo hakuna sababu nyingine za kuchelewesha kukamilika kwake", amesisitiza Waziri Prof. Mbarawa.

Vilevile Waziri Prof. Mbarawa amekagua uharibifu uliofanywa kwenye miundombinu ya taa za barabara katika Wilaya ya Urambo na





*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa akiangalia uharibifu wa miundombinu wa taa za barabarani katika Wilaya ya Urambo Mkoani Tabora. Kulia ni Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Tabora, Mhandisi Raphael Mlimaji.*

kuomba uongozi wa Mkoa wa Tabora kuchukua hatua stahiki kwa wananchi walioharibu miundombinu hiyo kwa kung'oa taa saba na kuisababisha Serikali hasara ya takriban Shilingi Milioni 21.

Aidha, Waziri Prof. Mbarawa ametoa wito kwa wananchi kutofanya shughuli zozote karibu na alama za mipaka ya barabara zilizowekwa kwani kufanya hivyo ni kosa kisheria na hatua kali zitachukuliwa.

Kwa upande wake Meneja wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Mkoa wa Kigoma, Mhandisi Ngoko Mirumbe, amesema Wakala utahakikisha mkandarasi anaongeza kasi ya ujenzi ili kutochelewesha kukamilika kwa mradi huo kwani unatakiwa kukamilika Oktoba mwakani.



*Muonekano wa sehemu ya barabara ya Malagarasi - Ilunde - Uvinza (km 51.1), inayojengwa kwa kiwango cha lami, Mkoani Kigoma.*

Naye Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), mkoa wa Tabora Mhandisi Raphael Mlimaji, amemuhakikishia Waziri Mbarawa kuwa TANROADS itamsimamia Mkandarasi anayejenga barabara ya Kazilambwa hadi Chagu ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na viwango walivyokubaliana katika mkataba.

Ujenzi wa barabara ya Malagarasi-Ilunde hadi Uvinza wenye kilomita 51.1 unaojengwa kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 17 na ujenzi wa barabara ya Kazilambwa hadi Chagu yenye urefu wa kilomita 36 unaojengwa kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 65.



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (wa pili kulia), akimsikiliza Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Tabora, Mhandisi Raphael Mlimaji, hatua za ujenzi wa barabara ya Kazilambwa - Chagu yenye urefu wa kilomita 36 inayojengwa kwa kiwango cha lami, Mkoani Tabora.*



*Muonekano wa hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa barabara ya Kazilambwa hadi Chagu (km 36) inayojengwa kwa kiwango cha lami Mkoani Tabora. Ujenzi wa barabara hiyo kwa sasa umefikia asilimia 65.*



# NCC WATAKIWA KUANDAA MIONGOZO BORA YA UJENZI.

Na **Segolena Francis -** WUU

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe.Atupele Mwakibete ameitaka Bodi ya Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), kuandaa Sera, Sheria, Kanuni na miongozo bora itakayosimamia na kuleta maendeleo ya sekta ya ujenzi nchini.



*Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Atuple Mwakibete (katikati), akimkabidhi makabrasha ya vitendea kazi Mwenyekiti mpya wa Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), Dkt. Fatma Mohamed (kushoto), mara baada ya kuzindua Bodi hiyo jijini Dar es Salaam.*

“

Naagiza zoezi hili lifanyike haraka, lakini kwa umakini na weledi kwa kuwashirikisha wadau wote ili kuleta tija inayotarajiwa,”

**amesema Mwakibete.**



*Mwenyekiti mpya wa Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), Dkt. Fatma Mohamed (kushoto), akionesha makabrasha ya vitendea kazi alivokabidhiwa na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Atuple Mwakibete (kulia), wakati wa uzinduzi wa Bodi hiyo jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Atupele Mwakibete (kulia), akiteta jambo na Naibu Katibu Mkuu wa Sekta ya Ujenzi, Ludovick Nduhiye (katikati), mara baada ya kuzindua Bodi ya Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), jijini Dar es Salaam.*

Akizindua Bodi mpya ya NCC jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri Mwakibete amesema maendeleo endelevu katika sekta ya ujenzi nchini yatapatikana endapo uwepo wa Sheria, Miongozo ya Majenzi, na Viwango Msawazo vya majengo na nyumba za Serikali vitakuwepo na kuzingatiwa na wadau wote wa sekta ya majenzi.

"Naagiza zoezi hili lifanyike haraka, lakini kwa umakini na weledi kwa kuwashirikisha wadau wote ili kuleta tija inayotarajiwa," amesema Mwakibete.

Aidha, ameitaka Bodi hiyo kuandaa miongozo ya gharama za ujenzi wa miradi ya barabara ili miongozo na sheria zote zitumike katika mwaka wa fedha ujao wa 2023/2024.

"Ninavyozungumza hivi sasa hatuna Sheria ya Majenzi, hatuna Miongozo ya Majenzi, hatuna Kanuni za Majenzi. Hivyo mtaona kwamba mnayo mambo mengi ambayo mnatakiwa kuyafanyia kazi kwa haraka ili kubadili mtazamo wa wadau na Serikali juu ya Baraza la Taifa la Ujenzi," alisisitiza Mwakibete.

Hata hivyo ameitaka NCC kufanya kazi kwa bidii ili kuleta ubunifu na tija katika sekta ya majenzi kwa ujumla.

" Sekta ya ujenzi katika nchi yoyote ni sekta muhimu kwa jinsi inavyochangia maendeleo ya uchumi wa nchi na kwa Tanzania sekta hii inachangia wastani wa asilimia 14 za pato la Taifa kwa mwaka,"amebainisha Naibu Waziri huyo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti mpya wa Bodi hiyo ya NCC Dakta, Fatma Mohamed amesema Bodi hiyo itafanya kazi kwa bidii na kuleta mabadiliko chanya kwa kuwa wajumbe wa Bodi hiyo ni wataalam waliobobea katika Sekta ya Ujenzi.

# HALMASHAURI YA MPIMBWE KUJENGEWA BARABARA YA LAMI.

Na **Deniza Cyprian** - WUU

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, ameelekeza ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Mlele (km 50), kwa kiwango cha lami uanze katika Makao Makuu ya Halmashauri ya Mpimbwe kwa ajili ya kusogeza huduma za usafiri na usafirishaji wa abiria na mazao.



*Muonekano wa sehemu ya barabara ya Kibaoni - Mlele (km 50) itakayojengwa kwa kiwango cha lami, mkoani Katavi. Ujenzi wa barabara hiyo utagharimu Shilingi Bilioni 88.*

Prof. Mbarawa, ametoa agizo hilo mkoani Katavi, wakati alipokagua ujenzi wa mradi huo ulioanza kutekelezwa na mkandarasi China Railways Seventh Group na kusimamiwa na Kitengo Maalum cha Wahandisi Washauri (TECU) kwa gharama ya shilingi Bilioni 88 ambao utatekelezwa kwa muda wa miezi 36.

"Kikawaida Barabara inaanza kujengwa walipo wananchi na tumeshakubaliana na TANROADS mkoa kuwa wataanza kwa kuunganisha makao makuu ya halmashauri kwani kuna shughuli mbalimbali za kibinadam zinaendelea", amesisitiza Prof. Mbarawa.

Prof. Mbarawa amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami na kufanikisha kuunganisha Wilaya ya Mlele na Mpanda ambapo kuna uzalishaji mwingi wa mazao ya mpunga, ufuta na mahindi.

Amewahakikishia wananchi wa Wilaya ya Mlele kuwa ujenzi wa barabara hiyo utakamilika kwa ubora unaotakiwa na kusisitiza kuwa mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2025.

Prof. Mbarawa ameahidi wananchi wa Mlele kupata ajira nyingi katika mradi huo na kuwaomba wale watakaopata fursa hiyo kuwa waaminifu na kuhakikisha wanatoa ushirikiano wakutosha kwa mkandarasi na kutohujumu mradi.

"Hii barabara ni yenu na mmeisubiri kwa muda mrefu sasa itakuwa jambo la ajabu kwa wale watakaopata kazi hapa kuanza kuiba mafuta au saruji, Tunataka barabara hii idumu kwa muda mrefu kama ilivyofanyiwa usanifu, hivyo tutunze vifaa na kushirikiana vyema na mkandarasi", amefafanua Prof. Mbarawa.

Naye, Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Katavi, Eng. Martin Mwakabende amemueleza Waziri huyo kuwa mradi huo unahusisha usanifu wa kina pamoja na ujenzi na hatua zinazoendelea hadi sasa ni kwamba mkandarasi amekwishaleta mitambo eneo la kazi na kazi imeanza ya kusafisha barabara.

Ameeleza ujenzi wa kambi ya mkandarasi umekamilika kwa asilimia 100 na ujenzi wa kambi ya Mhandisi Mshauri na Maabara bado inaendelea.

Waziri Prof. Mbarawa yupo mkoani Katavi ambapo amekagua miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wizara ikiwemo miundombinu ya barabara.



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akimsikiliza Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mkoa wa Katavi, Eng. Martin Mwakabende, kuhusu hatua ya ujenzi wa barabara ya Kibaoni - Mlele Junction (km 50), kwa kiwango cha lami, Mkoani humo.*



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akitoa maelekezo kwa Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mkoa wa Katavi Eng. Martin Mwakabende (kulia), wakati ujenzi wa barabara ya Kibaoni - Mlele Junction (km 50), kwa kiwango cha lami, Mkoani humo.*

# KIKAO CHA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU.

Na **Mwandishi Wetu** - WUU



*Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya akitoa taarifa ya utendaji wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), na Bodi ya Usajili ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), kwa kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu, jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mhe. Seleman Kakoso, akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, wakati wa uwasilishaji wa taarifa ya utendaji ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Bodi ya Usajili ya wabunifu Majengo na wakadiriaji Majenzi (AQRB), jijini Dodoma*







*Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, wakifuatilia taarifa ya Utendaji ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Bodi ya Usajili ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), ilipowasilishwa kwa kamati hiyo, jijini Dodoma.*

# UJENZI NA UCHUKUZI, WASHIRIKI SHIMIWI TANGA 2022.

Na **Mwandishi Wetu** - WUU







*Wanamichezo kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wakipita mbele ya Mgeni Rasmi Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala bora, Mhe. Jenista Mhagama, (hayupo pichani) wakati wa ufunguzi wa mashindano ya Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), Jijini Tanga.*




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala bora, Mhe.Jenista Mhagama akizungumza na baadhi ya wanamichezo wa Sekta ya Uchukuzii, mara baada ya Ufunguzi wa Mashindano ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), jijini Tanga.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala bora, Mhe. Jenista Mhagama akizungumza na Mwalimu wa kamba kutoka Sekta ya Uchukuzi Bw.Nicas Luanda, mara baada ya kufungua Mashindano ya michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), ambapo Uchukuzi ilishinda Roundi zote mbili dhidi ya Wapinzani wao Hazina, Jijini Tanga.*






*Wachezaji wa Timu ya Kuvuta Kamba Kutoka Sekta ya Uchukuzi, (wenye sare ya bluu) wameibuka kidedea mara baada ya kuwafunga timu ya Hazina kwa kuwavuta raundi zote mbili, mchezo ulioshuhudiwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala bora, Mhe. Jenista Mhagama, wakati wa ufunguzi wa Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), Jijini Tanga*



# HAFLA YA UWEKAJI JIWE LA MSINGI KIWANJA CHA NDEGE CHA KIMATAIFA CHA MSALATO.

Habari Picha



*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Rosemary Senyamule, Naibu Katibu Mkuu CCM Bara Christine Mndeme, Mwakilishi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika Dr. Patricia Laverley na Katibu Mkuu (Ujenzi), Balozi. Eng. Aisha Amour katika picha ya pamoja wakati wa hafla ya uwekaji jiwe la msingi ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato jijini Dodoma.*

*picha ya chini kulia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mhe. Seleman Kakoso*





Katibu Mkuu (Ujenzi), Balozi. Eng. Aisha Amour na Mwakilishi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika Dr. Patricia Laverley (kulia), wakiteta jambo.





Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, Mwakilishi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika Dr. Patricia Laverley, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Rosemary Senyamule na Naibu Katibu Mkuu CCM Bara Christine Mndeme wakiteta jambo wakati wa hafla ya uwekaji jiwe la msingi ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato jijini Dodoma.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa na Mwakilishi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika Dr. Patricia Laverley na Viongozi wengine wa Serikali kabla ya kukata utepe kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, jijini Dodoma.



Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Mwigulu Nchemba (wa kwanza kulia) katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato jijini Dodoma.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Atupele Mwakibete (kulia) akisalimiana na Mtendaji Mkuu wa TANROADS Eng. Rogatus Mativila wakati wa hafla ya uwekaji jiwe la msingi ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato jijini Dodoma.



Wataalam wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi wanaohusika na masuala ya ujenzi wa viwanja vya ndege mara baada ya hafla ya uwekaji jiwe la msingi ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato jijini Dodoma.



*Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Atupele Mwakibete (kulia) akisalimiana na Mkurugenzi wa Miradi wa TANROADS Eng. Boniface Mkumbo wakati wa hafla ya uwekaji jiwe la msingi ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato jijini Dodoma.*



*Baadhi ya Watumishi wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato jijini Dodoma.*





**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi**
**Mji wa Serikali Mtumba**
**S.L.P 2888 Ujenzi / S.L.P 638 Uchukuzi**

## DODOMA

**Simu: +255 26 23244455 / +255 26 2322703, 2322702**
**Nukushi: +255 26 2323233 / +255 26 2322704**
**Barua pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwt.go.tz**

wizarayaujenzinauchukuzi
wizaraUJnaUC
www.mwt.go.tz